# KUPAMBANUA MAWAZO YAKO KWA NENO LA MUNGU

*Waebrania 4:12:13 – kwa maana neno la Mugnu li hai tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upmga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafasi na roho na viungo tena lijepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo*.

Ndugu Branhan tafadhali elezea ni kwa namna gani mtu anaweza kujua kama anawaza mawazo yake mwenyewe au kama shetani ameweka mawazo yake katika nia yake kumfanya yeye awaze yasiyosahihi hasa kama anajua hataki kuyawaza hayo.

Angalia kama ni kinyume na Neno, hayo ni mawazo ya Shetani. Kama yanakubaliana na Neno, hayo ni mawazo ya Mungu. Kama ni mawazo yasiyo sahihi hayo, hayo ni shetani. Kama ni mawazo mazuri ya Neno na ni la Mungu, hayo ni mawazo ya Mungu.

Nabii wa kizazi chetu aliulizwa tena: Kama ni shetani pengine anayeweka mawazo yake katika nia yako juu ya mambo fulani,utawezaje kuyashinda au kuyaondoa?

Chukua kinyume kabisa na hayo. Kama shetani anakufanya ufikiri kuwa wewe ni……………Kama unajua wewe ni mkristo, na anajaribu kukufanya ufikiri kuwa wewe sio mkristo, wewe chukua tu kinyume chake, sema mimi ni mkristo ’’ili mradi maisha yako yanalingana na Neno la Mungu sema,’’Mimi ni Mkristo’’.Kitu kingine chochote ni hivyo hivyo. [1]

Kristo ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, masihi aliyepakwa mafuta. Mwaminio anashikilia hilo Neno. Mungu na Neno lake ni mmoja. Mimi na Neno langu tu mmoja. Wewe na neno lako ni mmoja. Sasa usiegemee kutumia mawazo yako mwenyewe, tumia mawazo Yake, hapo sasa wewe ni sehemu na Mungu kwa sababu Neno lake na wewe vimekuwa sawa, unaona? Hapo sasa uko katika ufalme. [2]

Hapo sasa sisi ni Neno la Mungu lililodhihirishwa.

Hivyo ndivyo mungu anavyolitaka Kanisa lake ni ili Yeye ajidhihirishe mwenyewe. Atawezaje kujidhihirisha Mwenyewe mpaka mbegu Yake Mwenyewe iwe ndani ya huyo mtu? Wawezaje kutumia mawazo yako mwenyewe na Mungu ajidhihirishe mwenyewe kupitia wewe? [3]

Lakini hivyo ndivyo hasa Mungu anavyohitaji kuacha vyote na kumfuata Yeye. Hilo ndilo Mungu analohitaji. Inatupasa kufanya hivyo pia. Wakati mwingine inabidi tuache mawazo yetu wenyewe. Kama mawazo yetu yako kinyume na Neno la Mungu, inabidi tuache, na kumfuata Yeye .na njia pekee tunayo weza kumfuata Yeye ni kufuata Neno lake na kulitii hilo. Na Mungu anavyo tuambia, na Mungu anavyohitaji ni kuwa, tuache vyote na kumfuata Yeye. [Luka 9;23]

Sasa kama Mungu Yule alieandika Biblia yuko ndani yako wewe sio mwenyewe [Galatia 2:19-20]. Umekufa katika mambo ya dunia. Umekufa katika mawazo yako. Na nia iliyokuwa ndani ya Kristo iko ndani yako, hapo sasa umeacha vyote na kumfuata Yeye. Siyo mawazo yako mwenyewe, Kile asemacho Yeye siyo mapenzi yangu mapenzi yako Bwana.”[Mathayo 26:36-42]. Hapo sasa unaanza kukaa kwenye mstari na Neno la Mungu.

Itabidi ufe .Inabidi ufe kabla hujazaliwa. Mbegu yoyote inabidi ife kabla haijajizaa tena. Ni mpaka ife kwanza sivyo itabakia peke yake [Yohana12:24]. Mtu inabidi afe katika mawazo yake mwenyewe. Inabidi afe katika mawazo yoyote yale, yabaki Maneno ya Mungu na aje kwenye njia Yake. Huo ndio uwanja wa Mungu. Hatukutani katika mawazo yetu. Tunakutana

Naye katika lile alilo agiza tufanye. Hiyo ndiyo njia Mungu aliyoiweka kwa ajili yetu. Watu wanaikwepa hiyo, hawaihitaji lakini ndio kweli hivyo hivyo. Inaleta mauti na inabidi ufe, ufe katika mawazo yako.

“Vema ninajua Biblia inasema hivyo, lakini siwezi kuielewa hivyo.” Hapo sasa kaa mpaka Mungu aifunue hiyo. Hiyo ni sawa. Huko ndiko kuzaliwa kwa pili [5]

Na inawapasa kuwa na kule kusulubishwa kabla ya kuwa na ufufuo (Galati 6:14) na kabla ya kanisa kuweza kuona nguvu za kufufuka, kabla mimi sijaweza kuona huduma mpya ikifanya kazi, kabla hujaweza kuingia katika ushirika mpya na Mungu, lazima kuwe na kujisulubisha mwenyewe ili kwamba kuweze kwa na kufufuka. Imetupasa Kufa kabisa katika mawazo yetu, kufa katika njia zetu, tufe kabisa kaika kila kitu kinachotuzunguuka, kuingia katika majaribu na mateso, hayo yote ni ili tuone ufufuo mpya, maisha mapya. Kabla ya mwenye dhambi hajaweza kuwa mkristo, lazima kuje mauti halafu ufufuo. [6]

Sasa kama tunaweza kujisalimisha sisi wenyewe kikamilifu kwa Mungu na mapenzi Yake na kupotea kabisa kwenye mawazo yetu, na kuachia tuu Nia ya Kristo iwe ndani yetu (Wafilipi 2:5), Utendai uleule wa Roho Mtakatifu utatenda kazi kupitia sisi, kama vile tuu mambo ya asili yafanyavyo, ni jambo lilelile. Kwa sababu kule mwazo tuliumbwa kwa kusudi hilo la kuongoza, kutawala na kumtukuza Mungu, na kuishi kwa aili ya Mungu.

Sasa Yesu alisema Sasa ''Ninyi mlikaa ndani yangu na Maneno yangu yakikaa ndani yenu, Ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa . Ninyi mlikaa ndani yangu na maneno yangu ndani yenu…''(yohana 15:1-7).

Sasa, Baba na Neno lake havitenganishiki kwa sababu Neno ni Mwana wake.''Hapo mwanzo kulikuwako Neno Naye Neno alikuwako kwa Mungu . .Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu ''Yohana 1:1-14). Mungu na Neno lake havitenganishiki. Huwezi ukawa na Mungu bila kuwa na Neno lake na unapokuwa na Neno lake una Mungu . [7]

Sasa jambo la kwanza unalopaswa kufanya ni kujisalimisha mwenyewe kikamilifu kwa Kristo, na kusalimisha mawazo yako kwa Neno lake. “Bwana, sitatenda kama ninavyo jisikia mwenyewe, wala juu ya mawazo yangu. Nitatenda tuu kulingana na Neno lako. Sitajiongoza mwenyewe kwa mawazo yangu juu ya hilo” [8]

Vema, kwa hiyo waaminio wa Neno na Roho lazima wawe mmoja. Unalipata hilo? Waaminio, Neno na Roho kwa hakika wao ni mmoja .Hufanyi kuwaza mawazo yako mwenyewe, hutumii mawazo yako mwenyewe. Je hilo si la ajabu? Ile nia iliyokuwa ndani ya Kristo iko ndani yako,wewe ni Neno. Wewe ni Neno la Mungu liishilo, muwakilishi wake hapa duniani (2kor.5:20) ukiziendeleza zile kazi. Kanisa linapaswa kuwa hivyo.

Na inapokuwa hivyo, ile Biblia inadhihirishwa tena kama ilivyokuwa kule sikuza mwanzo za wanafunzi.

Biblia inaishi tena ndani yako [3]

Sasa unajua, ninayo furaha sana kujua kuwa ipo njia tuliyopewa. Unaona, zipo njia mbili tuu kwa kitu chochote.kwamba kuna njia sahihi na njia ya makosa .Na hiyo ni njia yako na njia ya Mungu. Huwezi (ukawa) kuchukuwa njia yako na uwe kwenye njia ya Mungu, na huwezi kuwa katika njia ya Mungu na uchukue njia yako. Unaona? Kwa hiyo inabidi uchukue moja au nyingine. Itabidi uchukue njia yako au ya Mungu.Ni mawazo yako au Neno la Mungu. Unaona inabidi ukubali moja. Huwezi ukachukuwa

mawazo yako kwa kuwa mtu amezaliwa akiwa aliyeshindwa, na siku zote amekuwa aliyeshindwa. kwa hiyo ni kwa nini utegemee uelewa wako mwenyewe? Kwa nini usichukue njia ya Mungu kwa (jambo) hilo? kwasababu siku zote amekufanya utokee kuwa sahihi. [9]

Kwa sababu ukumbuke; huwezi kuwa na mawazo/ nia ya Kristo na mawazo/nia ya dunia kwa wakati mmoja. Hwezi ukawa kwenye njia yako na njia ya Mungu kwa wakati huo huo. Inabidi uondoke kwenye njia yako ili Mungu achukue njia Yake. Hiyo ndiyo njia pekee itakayo kuwezesha kufanya chochote. Inabidi uende mbali na mawazo yako, hoja zako mwenyewe, (mithali 3:5-6). Usijaribu kuhoji uamini tuu. (2kor 10:3-6)

Ingekuwaje kama Maria angehoji juu ya uzazi wa kibikira, ni vipi kama angejaribu kusema sasa subiri kwa dakika/kidogo. Sasa angalia sijui mtu yoyote jambo hilo kamwe halijawezekana kwa mtu yoyote kama hivyo. Nawezaje mimi kuwa na mototo? Oh huwezi ukaniambia mimi hivyo kamwe. Hakusubiria chochote (Maria) alimchukuwa Mungu katika Neno lake na kuanza kumshukuru Mungu kwa ajili ya mototo. Kabla hajasikia uhai wowote, kabla hajasikia chochote, kabla hajapewa ishara yoyote, yeye (Maria) alichukua Neno la malaika na alienda akifurahia na kumsifu Mungu akimwambia kila mtu kuwa atapata mototo akiwa hajui mume. Mungu utupe akina Maria wengi kuzunguka hapa FOENIKSI, ambao wanaweza

kumchukuwa Mungu kwenye Neno lake na kuanza kufurahia kabla chochote hakijafanyika. Hicho ndicho unachohitaji, hivyo ndivyo ilivyo hasa kwa maana alifunikwa na Roho Mtakatifu (Luka 1:26 - 56) na ni Roho Mtakatifu akimfunika mtu kweli, wanamchukuwa Mungu katika Neno lake hivyo inamaliza hilo, kile Roho Mtakatifu alichosema [10]

Sasa wakati ile nuru ilipommulika Rebekah mdogo alijua kitu fulani ndani yake, kilekile kilichomleta kwa ishara, alifunika uso wake, hakutaka chochote kile kuhusu mawazo yake. Ishara ndio ilikuwa mawazo yake kuanzia hapo. (mwanzo 24). Na kanisa lenyewe linapoguswa na zile nguvu za Mungu ule ubatizo wa Roho Mtakatifu kutoka kule kwa kanisa la kidhehebu kutoka kule kwa kanisa katoliki popote lilipo wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu unapofanywa kuwa halisi kwa watu wale waliochaguliwa kimbele kwa uzima wa milele unaona hilo na kutembea katika hilo. Na nini hiyo? Ishara kuu [11]

Sasa hapo huwazi mawazo yako, unatumia mawaza Yake ”Iweni na nia hiyo hiyo iliyokuwa ndani ya Kristo” (wafilipi 2:5) unaona? Fikiria njia yake ya kufikiri, sema anachosema “kuungama” maana yake ni kusema jambo lile lile” kuungama ni kusema jambo lile lile sasa usifikiri mawazo ya uelewa wako wa kiakili. Uzaliwe mara ya pili na ukiri Neno lake. Kiri kile alichosema, huko ni kuungama sema kwa kupigwa kwake mimi niliponywa (Isaya 53:5) kwa kupigwa kwake ninayo haki kwa vidonda vyake, sasa hivi ninayo haki ya wokovu ninayo haki kwa Roho Mtakatifu, aliahidi hilo kwangu alisema “ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu na kwa watu wote walio mbali na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie (Matendo 2:38 - 39) [12]

Nukuu za kingereza.

[1] Maswali na majibu (64-0830E)swali no 387+388 COD ule 1158-1159.
[2] “Kuporomoka ka dunia(62-1216),aya 118
[3] Lile neno lililonenwa ndiyo mbegu ya asili (62-0318),ule 28+42
[4] Kuyaacha yote (62-0123),aya E32,E 37
[5] Njia Mungu aliotupa kwa siku hii ya leo(64-0206E) Aya 28 +42
[6]Ninajua (60 - 04175) Aya 61
[7] Misingi ya mwanzo ya Imani (55 0113) aya E 14
[8] Mkono wa Bwana umefunuliwa nani? (50 - 0824) aya E 42
[9] Mungu anayo njia aliyoiweka (62 0728) aya E 11
[10] Mashahidi (54 0303) aya E 27 E 28
[11] Ishara kuu (62 0708) aya 140
[12] Kristo (55 - 0221) aya E 49

---

Jiwe la kujengea la kiroho nambari 108 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendestr. 69.D-75328 Schomberge Germany Simu (+49) 2357613 Fax 72353306.

---

*Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk.724)*

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa: Charles E. Y. Kanju

*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*